
Editon Consortium Journal of Kiswahili [ISSN: 2663 - 9289]




**Issue no:** 1 | **Vol no:** 5 | **April** 2024: 11-20

# Uhalisia mazingaombwe kama mbinu ya mtindo wa uandishi wa ubaadausasa katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) ya S. A. Mohamed

**Mary Njambi Muigai**[(1)]
**Issa Y Mwamzandi**[(2)]
**Robert W Oduori**[(3)]

(1.3) Chuo Kikuu cha Moi, Kenya; (2) Chuo Kikuu cha Kabianga, Kenya.
Main author email: marynjambi06@yahoo.com

**Article History**
Received: 2024-01-02
Accepted: 2024-03-08
Published: 2024-04-24

**Cite this article in APA**
Muigai, M. N., Mwamzandi, I. Y., & Oduori, R. W. (2024). Uhalisia mazingaombwe kama mbinu ya mtindo wa uandishi wa ubaadausasa katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) ya S. A. Mohamed. *Editon consortium journal of Kiswahili*, *5*(1), 11-20. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v5i1.480

**Ikisiri**
Makala haya yamejadili matumizi ya uhalisia mazingaombwe kama mbinu ya mtindo wa uandishi wa ubaadausasa katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010) ya S. A. Riwaya hii imedhihirisha upya kwa kukaidi mtindo wa uandishi wa kimapokeo ukiojikita katika uhalisia, na kugeukia mtindo wa uandishi wa kibaadausasa. Makala haya yanachunguza matumizi ya uhalisia mazingaombwe katika riwaya hii, kama kipengele mojawapo cha mtindo wa uandishi wa ubaadausasa. Lengo kuu la makala haya ni kubainisha vipengele vya uhalisia mazingaombwe na namna vimetumika katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*. Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Ubaadausasa inayopendekeza uanuwai wa mawazo kwa kukaidi kuwepo na mtazamo mmoja wa kueleza tajriba tofauti za binadamu, au simulizi kuu. Sampuli dhamirifu ilitumika kuteua riwaya ya hii. Data ilipatikana kupitia usomaji wa kina wa riwaya. Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya Nadharia ya Ubaadausasa na kuwasilishwa kwa maelezo ya kinathari. Matokeo yalibainisha kwamba riwaya hii iliziba mipaka kati ya uhalisia na umazingaombwe kupitia matumizi ya wahusika binadamu wenye nguvu za ajabu kama vile kuwasoma watu. Aidha, riwaya hii ilitumia viumbe wa ajabu kama vile mizuka, vivuli, majini na wafu kuwakilisha hali halisi ya dunia ya sasa ambayo imejaa mambo mengi ya ajabu yasiyoelezeka. Katika kutamatisha, ilibainika kuwa matumizi ya uhalisia mazingaombwe ni mbinu ya kiumbuji anayotumiwa mwandishi kukaidi simulizi kuu ya uandishi wa kimapokeo wa riwaya ya Kiswahili uliojikita katika uhalisia. Matumizi ya mtindo huu ni dhihirisho la mabadiliko katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili.

**Maneno muhimu**: Simulizi kuu, ubaadausasa, uhalisia, uhalisia mazingaombwe.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Kuzuka kwa mtindo wa uandishi wa ubaadausasa kumeleta mabadiliko makubwa katika uandishi wa fasihi ya Kiswahili, hususan riwaya. Mtindo huu ulianza kuwa maarufu miaka ya sitini katika nchi za kimagharibi (Lewis, 2001). Hata hivyo, mtindo huu umeanza kutumika katika fasihi ya Kiswahili katika mwongo wa mwisho wa karne ya ishirini kama njia ya kuonyesha mabadiliko yanayotokea katika dunia ya sasa hasa kutokana na utandawazi (Khamis, 2005; Traore, 2014). Mtindo wa uandishi wa ubaadausasa unakaidi mtindo wa uandishi wa kimapokeo uliokuwa umezoeleka, na ambao ulijikita katika uhalisia. Katika misingi ya kihalisia lazima sanaa iaminike; matukio huakisi hali halisi ya maisha ya watu na usawiri wa wahusika husadiki maisha yao ya kila siku (Khamis, 2008). Vilevile, bunilizi zenye misingi ya kihalisia aghalabu hutumia wahusika watu ambao wanaweza kupatikana katika mazingira na hali halisi na hutambulishwa kwa majina halisi (Watt, 2000; Wamitila, 2002). Hata hivyo, riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* inatumia mtindo unaokiuka kaida hizi za kihalisia zinazosisitiza uyakinifu na mantiki katika kazi ya fasihi. Badala yake inatumia mtindo wa kimajaribio wa ubaadausasa unaojitokeza kupitia matumizi ya uhalisia mazingaombwe. Kama wanavyorai wataalamu mbalimbali (k.m. Mwamzandi, 2013; Waliaula, 2010; Khamis, 2007; D'haen, 2005) uhalisia mazingaombwe ni mojawapo ya vipengele vinavyotambulisha kazi za kibaadausasa. Ni bayana kuwa matumizi ya uhalisia mazingaombwe ni mbinu ya mtindo wa uandishi wa ubaadausasa anayotumia mwandishi wa riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* kukaidi uandishi wa kimapokeo uliokuwa umezoeleka uliojikita katika uhalisia.

Kwa mujibu wa Waliaula (2010) waandishi wa Afrika Mashariki waliotumia mtindo wa uhalisia mazingaombwe ni pamoja na S. A. Mohamed, K. W. Wamitila na E. Kezilahabi. Baadhi ya kazi za S.A. Mohamed zilizotumia mtindo huu ni *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010). Kati ya riwaya hizi tatu za S. A. Mohamed, riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ndio haijahakikiwa kwa kina sana kuhusu matumizi ya uhalisia mazingaombwe. Hilo ndilo pengo ambalo makala haya yanalenga kuziba kwa kujikita katika Nadharia ya Ubaadausasa.

## MAPITIO YA MAANDISHI

### Uhalisia na Sifa zake Bainifu

Kwa mujibu wa Senkoro (2011), kila utanzu huambatana na kanuni au mambo yanayojitokeza mara kwa mara katika uwanja husika. Katika riwaya, hususan riwaya ya Kiswahili, mtindo wa uandishi uliozoeleka ni ule wa kimapokeo na ambao ulijikita katika uhalisia. Waandishi na wahakiki tofauti kama vile Watt (2000), Wamitila (2002), Ntarangwi (2004) na Goring n.w. (2010) wanakubaliana kuwa uhalisia ni kipengele mojawapo ambacho wanamapokeo walitumia ili kuibainisha riwaya. Wamitila (2002:114) kwa mfano, anasema:

> Uchunguzi wa utanzu wa riwaya unaambatana na uhalisia kwa kiasi kikubwa hivi kwamba haiwezekani kuizungumzia riwaya bila ya kuyarejelea mawazo yanayohusishwa na uhalisia.

Maelezo ya Wamitila hapo juu yanabainisha kuwa uhalisia ndio ulikuwa msingi wa kuziandika riwaya za kimapokeo. Hivyo, ilibidi riwaya ziandikwe kwa kutumia mtindo wa uhalisia ili zikubalike kuitwa riwaya. Uandishi wa kihalisia uliandamana na sifa mbalimbali katika vipengele vyote vya fani kama vile ploti, wahusika, lugha, mandhari na urefu. Goring n.w. (2010) kwa mfano wanaeleza riwaya za kihalisia kama bunilizi iliyosimuliwa kwa lugha ya kinadhari na ambayo ina urefu wa kadri na ambapo wahusika na matendo yao huwakilisha hali halisi ya maisha yanayowasilishwa kwenye ploti sahili au changamano.

Forster (2002), Watt (2000) na Wamitila (2002) nao wanabainisha sifa zifuatazo za riwaya za kihalisia. Kwanza, katika riwaya za kihalisia wahusika, matukio na madhari yanapaswa kuoanana na uhalisia wa jamii husika. Kwa mfano, bunilizi hizi aghalabu hutumia wahusika watu ambao wanaweza kupatikana katika mazingira na hali halisi na hutambulishwa kwa majina halisi. Aidha, matukio na visa hupangwa kufuatia wakati na kwa njia ambayo chakula cha mchana huja baada ya chamsha kinywa, Jumanne baada ya Jumatatu, kuoza baada ya kifo na kadhalika. Mandhari nayo huwa ya kawaida au

yanayoweza kuonekana katika jamii. Kinachobainika katika sifa hizi ni kuwa uandishi wa kihalisia huwiana na ukweli wa jamii husika kwa upande wa mandhari, wahusika na matendo yao.

Wamitila (2002) vilevile anasema kuwa riwaya ya kihalisia hulenga kufikia tamati au hitimisho ambapo suluhisho la matatizo yaliyojadiliwa linapatikana mwishoni mwa riwaya. Lengo kuu la riwaya hizi huwa ni kupata suluhisho na kuthibitisha kwamba kuna mshikamano katika jamii na kumhakikishia msomaji kwamba mifumo ya maadili na itikadi za kitamaduni bado zina mashiko katika jamii husika. Aidha, fasihi yenye misingi ya kihalisia inafaa kufikiwa na kila mwanajamii na wala sio tu wasomi au watu wa tabaka la juu. Kwa hivyo, lugha ambayo hutumika pamoja na uteuzi wa msamiati unafaa kuelekea kwenye mtindo sahili. Ni bayana kuwa kazi za kihalisia zililenga kuhodhi ukweli kama tuujuavyo. Matukio yalipaswa kuakisi hali halisi ya maisha ya watu, huku usawiri wa wahusika ukiambatana na mantiki ya hali halisi ya maisha yao ya kila siku. Katika muktadha wa ubaadausasa, uhalisia unajitokeza kama simulizi kuu, au msingi wa kuifasili na kuiandika riwaya, ambao wanaubaadausasa hupinga.

**Uhalisia Mazingaombwe na Sifa zake Bainifu**

Kwa mujibu wa Salenius (2009) wahakiki hawajaweza kukubaliana kikamilifu kuhusu sifa bainifu za uhalisia mazingaombwe. Hata hivyo, kuna sifa ambazo aghalabu hurejelewa mara kwa mara kama vile kuwepo kwa mambo na matukio yasiyo ya kawaida na ambayo hukinzana na kaida zilizozoeleka za kuutazama na kuueleza uhalisia. Vipengele vya mambo halisi na vya kimiujiza huwasilishwa kwa pamoja kana kwamba vinawasilisha uhalisia, hivyo basi kuziba mipaka ya wazi kati ya vipengele hivi (Bowers, 2004; Waliaula, 2010). Riwaya zenye vipengele vya uhalisia mazingaombwe huwapa wahusika wao sifa za kifantasia kama vile uwezo wa kupaa na kuelea angani, uwezo wa baadhi ya wahusika wa kuweza kuwasoma wengine (telepathia), pamoja na uwezo wa kuunda au kubomoa vitu kwa nguvu za kiungu (Baldick, 2008). Aidha, uhalisia mazingaombwe hudhihirika katika bunilizi yoyote kupitia matumizi ya mizuka, jambo ambalo huwezesha kuwepo kwa muungano wa mambo au mifumo, ambao haungewezekana katika aina nyingine ya bunilizi (Zamora na Faris, 1995). Isitoshe, matumizi ya uhalisia mazingaombwe hudhihirika kupitia matumizi ya "vipengele vya ngano, hekaya na visasili katika riwaya za kisasa ili kuweza kuangazia maisha katika jamii ya kisasa (Baldick, 2008:194). Akieleza kuhusu waandishi wanaotumia mtindo wa uhalisia mazingaombwe Abrams (1999) katika Waliaula (2010:143) anasema hivi:

> Waandishi hawa husukanisha uhalisia uliochongwa kwa njia maalum katika ruwaza inayobadilikabadilika daima, huku wakiwakilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina sambamba na vipengele vya kifantasia na kindoto, na kwa kutumia mambo yanayotokana na visaasili na hekaya.

Kinachobainika katika dondoo hapo juu ni kuwa uhalisia mazingaombwe huchanganya vipengele vya uhalisia na umazingaombwe. Ukweli huu unaambatana na maelezo ya Bowers (2004) anayeeleza kuwa uhalisia mazingaombwe hujitokeza wakati vipengele vya mambo halisi, mambo ya kufikirika au ya kimiujiza huwasilishwa kwa pamoja kana kwamba yanawasilisha uhalisia.

Kutokana na mawazo ya wataalamu tuliowajadili hapo juu tunaweza kutamatisha kwa kusema kuwa uhalisia mazingaombwe hutumia vipengele vya uhalisia sambamba na vile vya kimazingaombwe, kifantasia au vya kindoto, au vipengele vinavyotokana na visaasili na hekaya za jamii fulani, hivi kwamba hakuna mipaka ya wazi kati ya vipengele hivi. Haya ni baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza katika riwaya ya S. A. Mohamed tuliyoijadili katika makala haya. Ukosefu wa mipaka kati ya mambo halisi na ya kindoto au kifantasia unaambatana na maelezo ya Baudrillard (1981) ambayo yametumika kama mojawapo ya mihimili ya Nadharia ya Ubaadausasa katika makala haya. Matumizi ya uhalisia mazingaombwe kama mtindo wa uandishi basi dhihirisho la ukiukaji wa kaida za uhalisia.

**Uhusiano kati ya Uhalisia Mazingaombwe na Ubaadausasa**

Wataalamu mbalimbali wakiwemo Mwamzandi (2013), Waliaula (2010), Khamis (2007), D'haen (2005) na Zamora na Faris (1995) wanakubaliana kuwa uhalisia mazingaombwe ni mojawapo ya mikondo katika mwondoko wa ubaadausasa. Akifafanua uhusiano uliopo kati ya ubaadausasa na uhalisia mazingaombwe, D'haen (2005) anaeleza kuwa baadhi ya sifa ambazo hubainisha matini za kibaadausasa pia hupatikana katika uhalisia mazingaombwe. Sifa hizo ni kama vile uanuwai au mseto wa vitu, mwingiliano matini, kuvuruga udhabiti wa wahusika na usimulizi, ufutaji wa mipaka kati ya vitu na hali tofauti pamoja na hali ya kutofuata kaida zilizozoeleka. Mwingiliano huu wa sifa huufanya uhalisia mazingaombwe kuwa tawi mahususi katika mwondoko wa ubaadausasa.

Pollheide (2003) na Goring n.w. (2010) nao wanasema kuwa mojawapo ya mhimili muhimu wa fasihi ya kibaadausasa ni kule kutokubaliana na wanamapokeo kuwa uhalisia ni kipengele muhimu cha kuifafanua riwaya. Haya yanaambatana na mawazo ya Lyotard (1979:81) akizungumza kuhusu wasanii wa kibaadausasa na kazi zao. Anasema hivi:

> Msanii au mwandishi huwa kama mwanafalsafa: matini anazoziandika na kazi anazozibuni haziongozwi kamwe na kaida zilizowekwa tayari…wala hatuwezi kuhusisha kazi au matini fulani na kategoria zinazojulikana tayari. Kwa hivyo, msanii au mwandishi anafanya kazi yake bila kuongozwa na kaida au sheria yoyote ile, ili aweze kuunda kaida za kile ambacho tayari atakuwa amekiandika.

Mawazo ya wataalamu hawa yanadhihirisha kuwa wanaubaadausasa hutumia uhalisia mazingaombwe kama njia mojawapo ya kukiuka kaida za wanamapokeo kuhusu maana ya riwaya. Wanatumia uhalisia mazingaombwe kuunda kazi zao bila kuongozwa na kaida za awali zilizojikita katika uhalisia. Na kama anavyosema Lyotard (1979) kuwa ubaadausasa husaili mamlaka ya simulizi kuu, vivyo hivyo uhalisia mazingaombwe husaili mamlaka ya uhalisia na hivyo basi kudhihirisha kuwa uhalisia mazingaombwe ni mtindo wa kiuandishi katika Nadharia ya Ubaadausasa. Ukiukaji wa kaida zilizozoeleka ndio mhimili mkuu katika Nadharia ya Ubaadausasa. Hali hii huufanya uhalisia mazingaombwe kuwa kipengele muhimu katika Nadharia ya Ubaadausasa.

Aidha, uhalisia mazingaombwe ni ishara ya mabadiliko katika uwanja wa fasihi kuambatana na maneno yafuatayo ya Lyotard (1979: xxiii) akieleza kuhusu dhana ya ubaadausasa:

> [Ubaadausasa] hurejelea hali ya utamaduni uliyopo kwa sasa ambao, tangu mwisho wa karne ya kumi na tisa, umebadilika na kubadilisha kaida zilizozoeleka za kutenda mambo katika uwanja wa sayansi, fasihi na sanaa.

Ni bayana kuwa fasihi, hususan riwaya ya Kiswahili ya karne ya ishirini na moja imedhihirisha mabadiliko mengi. Matumizi ya uhalisia mazingaombwe ni dhihirisho la mabadiliko hayo kama ilivyojitokeza katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*. Akizungumzia kuhusu riwaya mpya ya Kiswahili ya karne ya ishirini na moja Khamis (2005) anataja matumizi ya uhalisia mazingaombwe kama mojawapo ya vipengele vinayodhihirsha upya katika riwaya hizi. Ni dhahiri kuwa matumizi ya uhalisia mazingaombwe yameleta mabadiliko katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili kwa kukaidi mtindo wa uandishi wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia.

## MBINU ZA UTAFITI

Makala haya yametumia mwelekeo wa utafiti kithamana kukusanya na kuhakiki data. Usampuli wa kimaksudi ulitumika kuteua riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ya S. A. Mohamed. Riwaya hii ilidhihirisha upya kwa kukaidi mtindo wa uandishi wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia na kugeukia mtindo wa uandishi wa ubaadausasa. Data ilikusanywa kupitia usomaji wa kina wa riwaya husika. Vipengele vya uhalisia mazingaombwe vilivyojitokeza viliteuliwa kwa mbinu ya kimaksudi na kunakiliwa kwenye daftari. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa mujibu wa malengo ya makala haya na mihimili ya Nadharia ya Ubaadausasa. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa maelezo ya kinathari.

**Misingi ya Kinadharia**

Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Ubaadausasa inayohusishwa na mwanafalsafa, Jean Francois Lyotard (1979). Mchango wake unapatikana katika makala yake maarufu, *The Post Modern Condition: A Report on Knowledge.* Katika makala haya Lyotard anaeleza ubaadausasa kama hali ya kuzishiku simulizi kuu. Anatumia neno simulizi kuu kurejelea nadharia na mifumo ambayo hudai kuhodhi ukweli halisi, au kutoa maelezo bia ya namna tunavyopaswa kuutazama ulimwengu au kutoa suluhisho la matatizo yote ya binadamu. Makala haya yake yaliweka msingi wa kuhakiki na hatimaye kupuuzilia mbali simulizi kuu mbalimbali ambazo aliziona zikiwa kandamizi.

Simulizi kuu halisi ambazo Lyotard alizitilia shaka ni mfumo wa Umarx, mwondoko wa Usasa na mradi wa Mwamko wa Kitaaluma kwa kuwa mifumo hii haikuweza kutimiza malengo ambayo iliahidi. Kwa mfano, Lyotard anasema kuwa Umarx ulisisitiza kuleta ukombozi wa binadamu kutokana na minyororo ya ubepari. Hata hivyo, haukuweza kuleta uhuru na ukombozi ulioahidi na hivyo basi hauwezi kuaminiwa tena. Kwa mujibu wa Lyotard basi, simulizi kuu kama hizi zinapaswa kupuuzwa.

Lyotard na wanaubaadausasa kwa jumla wanashikilia wazo kuwa hakuna ukweli halisi (Sim, 2001; Barry, 2002). Wanakataa kuamini kwamba kunayo misingi isiyopingika au taratibu maalum za kutenda jambo. Wanashuku simulizi kuu zinazodai kuhodhi ukweli halisi usioweza kupingika. Simulizi hizo ni kama vile umuundo, elimu, dini na utamaduni (Sim, 2001; Barry, 2002; Rivkin & Ryan, 2004). Katika makala haya neno simulizi kuu limetumika kurejelea nadharia ya uhalisia ambayo ilitumiwa na wanamapokeo kama msingi wa kuifasili na kuiandika riwaya, hususan riwaya ya Kiswahili.

Kwa kuwa wanabaadausasa huzipuuza simulizi kuu, Lyotard (1979) anapendekeza matumizi ya simulizi ndogo ndogo. Lyotard alieleza simulizi ndogo kama vikundi vya muda vya watu vilivyopaswa kusaili na kurekebisha ukandamizaji ulioenezwa na simulizi kuu. Kuambatana na mantiki hii, makala haya yamechukulia simulizi ndogo kama njia mbadala za kuiandika na kuifasili riwaya. Mtindo wa uandishi wa ubaadausasa unaweza kuchukuliwa kama njia mbadala ambayo S. A. Mohamed ametumia kukaidi mtindo wa kimapokeo, kwa kuingiza vipengele vya umazingaombwe katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*. Kama anavyosema Khamis (2005), waandishi katika karne ya ishirini na moja wanautumia mtindo huu kuuelezea ulimwengu wa sasa kwa njia njia ambayo uhalisia haukuweza kueleza.

Aidha Lyotard (1979) anasema kuwa hakuna sheria bia inayofaa kuongoza mawazo yetu. Anazua dhana ya 'tofauti' kupinga mifumo yoyote ambayo huleta hali ya kujumuisha tajriba tofauti za binadamu badala ya kuzingatia tofauti anuwai zilizoko. Kwake Lyotard, kutokubali kuwepo kwa tajriba tofauti kunaleta dhana ya ukandamizaji. Kama wanavyosema Deleuze na Guattari (1972), wanaubaadausasa wanajali na kusherehekea 'tofauti' na 'uanuwai' katika tajriba tofauti za binadamu wala si mshikamano. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* wazo hili la 'tofauti' limedhihirika kupitia mtindo wa uandishi mpya wa kibaadausasa ambao ni tofauti na uandishi wa kimapokeo. Mtindo huu unahusisha vipengele umazingaombwe ambavyo havikuwepo katika uandishi wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia.

Mawazo mengine muhimu katika makala haya ni yale ya mwanaubaadausasa Jean Baudrillard (1981). Katika makala yake *Simulacra* and *Simulation*, Baudrillard anachunguza uhusiano uliopo kati ya uhalisi na ishara katika ulimwengu wa kiteknolojia. Baudrillard anavishambulia vyombo vya vya kisasa vya kiteknolojia kwa kuwa havibainishi tofauti kati ya ishara na uhalisi. Anaueleza ulimwengu wa ubaadausasa kama ulimwengu wa maigizo na uigaji au *Simulacra* na *Simulation*, ambapo hatuwezi kubainisha tofauti kati ya uhalisi na wigo au ishara kwa kuwa tumezipa ishara umuhimu sana. Mwingiliano kati ya uhalisia na ishara au wigo ndio msingi wa kuhakiki matumizi ya uhalisia mazingaombwe katika makala haya. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* wahusika na matukio yamechanganya vipengele vya uhalisia na umazingaombwe ili kuunda kazi moja kamilifu ya kibaadausasa. Kwa mfano, inatumia wahusika halisi lakini wenye uwezo uliopita mipaka ya binadamu wa

kawaida. Katika kufanya hivyo, riwaya hii inaziba mipaka kati ya uhalisia na umazingaombe.

## MATOKEO

Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* imedhihirisha upya kutokana na matumizi ya vipengele vya uhalisia mazingaombwe kama dhihirisho la mtindo wa kipekee wa uandishi wa kibaadausasa unaokaidi uandishi wa kihalisia.

### Binadamu wa Kawaida wenye Uwezo wa Kiajabu

Mojawapo ya sifa za umazingaombwe hujikita katika uwakilishaji wa wahusika kwa kutumia binadamu wa kawaida wenye uwezo wa kiajabu. Uwakilishaji huu umejitokeza katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ambapo binadamu wa kawaida wamepewa uwezo wa kuwasoma na kuwajua wahusika wengine bila kutumia hisia za kawaida kama vile kuona, kugusa, kunusa na kadhalika. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* mhusika Nana anawaingia na kuwasoma washindani wenzake waliokuwa wamefika kwa mashindano ya waimbaji chipukizi katika mkahawa ulioitwa *Hoteli Selwa* (uk. 140-141). Nana anadhihirisha uwezo usio wa kawaida wa kuingia ndani ya wahusika wengine na hata kuzisikia sauti zao zikiimba licha ya kuwa wahusika hao hawakufungua vinywa vyao kuimba. Aidha, anapousikiliza uimbaji wao ana uwezo wa kuujua ufundi walionao na kuelewa bayana kuwa hakuna hata mmoja ambaye angeweza kumpiku. Inavyobainika pia ni kwamba sio wahusika wote walio na uwezo kama huu wa Nana. Kwa mfano, Nana anasema kuwa washindani wenzake hawakuweza kumjua au kumsoma, lakini yeye aliwaingia na kuwasoma wote waliokuwepo. Ingawa Nana anaonekana kama binadamu wa kawaida, uwezo huu wake unadhihirisha uhalisia uliochanganywa na umazingaombwe katika muktadha mmoja hivyo kufuta mipaka ya wazi kati ya hali hizi mbili, ambayo ni sifa mojawapo ya ubaadausasa.

Hali nyingine ya umazingaombwe inahusu uwezo wa baadhi ya wahusika wa kuona na kubashiri mambo ambayo yangekuja kutendeka baadaye kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Nani kwa hivyo, ndani ya nyumba hiyo asiyetambua uwezo wa Bi. Mau wa kuona visivyoonekana? Au nani aliyeweza kuthubutu uwezo wake wa kutabiri yasiyotabirika? Mara ngapi hapo nyuma yeye alikwisha tambua kuwa siku moja kitukuu chake kingerejea kuishi kwao licha ya Bw. Hila kikizuia kisikaribie nyumbani humo. Na leo si hiki kitukuu chenyewe kimekuja… (*NZM* uk. 174).

Tunaelezwa kuwa Bi. Mau alibashiri kuwa siku moja angeishi na kitukuu chake kilichoitwa Nana, jambo ambalo lilikuja kutimia. Uwezo huu wa Bi. Mau unadhihirisha umazingaombwe kwa kuwa umepita uwezo wa binadamu wa kawaida.

Mbali na kuwa Nana na Bi. Mau ni wahusika wenye mashiko ya uhalisia, wana uwezo wa kusafiri masafa marefu katika ulimwengu wa kiroho, ingawa miili yao haibanduki mahali ilipo katika hali halisi. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa wako nyumbani kwao lakini wanasafiri katika ulimwengu wa kiroho hadi chumba cha kulala cha Mwanamkuu na hata kuanza kuwasiliana naye (uk. 178-179). Uwezo huu wa Nana na Bi. Mau umepita mipaka ya uhalisia kama tunavyoujua, na hivyo kuingia katika tapo la uhalisia mazingaombwe. Mbali na kukaidi uandishi wa kihalisia, uwezo wa Bi. Mau na Nana unafuta mipaka kati ya uhalisia na umazingaombwe kwa kuwa mwandishi ametumia uhalisia unaoenda sambamba na umazingaombwe. Haya yanaambatana na mojawapo ya mihimili ya Nadharia ya Ubaadausasa kama ulivyofafanuliwa na Baudrillard (1981) anayerai kuwa kazi za kibaadausasa kufuta mipaka kati ya mambo halisia na yale yasiyo halisia.

### Matumizi ya Wahusika na Matukio ya Ajabuajabu

Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* imetumia wahusika wa ajabu ajabu kama vivuli, mizuka, vizuu, majini na wafu. Wahusika hawa wanatumiwa kuwakilisha binadamu halisi katika ulimwengu halisi lakini kwa njia iliyokiuka uhalisia. Vivuli sio watu walio na mwili kama binadamu wa kawaida, namna ambavyo wahusika katika riwaya za kihalisia wanavyohitajika kuwa. Badala yake hawa ni wahusika wa kuhisika tu lakini wanaowakilisha hali halisi ya maisha. Bi. Mau na Nana kwa mfano, wanaweza kuona na hata kuwasilisana na vivuli katika ulimwengu wa kiroho. Tunaelezwa kuwa wanapatana na vivuli vya

Mwanamkuu, Hawa na Maskati. Vivuli hivi vinalalamika kwa sababu ya dhuluma wanazozipitia kwa sababu ya jinsia yao, kama vile kubakwa, ndoa za kulazimishwa na kutalikiwa bila sababu. Katika ulimwengu huu wa kiroho, watu halisi kama Nana na Bi. Mau pia wanabadilishwa na kuwa vivuli ili waweze kuwasiliana na vivuli vyenzao. Kwa mfano, tunapata mawasiliano kati ya vivuli vya Nana, Bi. Mau na Hawa, baada ya kitoto cha Hawa kuuawa kinyama, kwa sababu kilizaliwa nje ya ndoa. Nana na Bi. Mau wanajaribu kumtuliza Hawa baada ya kitendo hiki cha kikatili:

> "Nyamaza… Nyamaza…" Kivuli cha Nana na cha Bi. Mau vilikipoza kile kivuli cha Hawa kwa huzuni.
> "Mpaka lini?" Kiliuliza kivuli [cha Hawa] ndani ya kilio na kwikwi.
> "Mpaka kila mtu atakapofahamu, mpaka sheria zitakaposimamishwa kututetea na kutulinda," kivuli cha Nana kilihakikisha (*NZM* uk. 180).

Kama inavyojitokeza katika dondoo, vivuli vinahuishwa na kupewa uwezo wa kibinadamu kama vile kulia na kuongea. Huu ni uhalisia unaoenda sambamba na umazingaomwe ambao unakaidi uandishi wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia. Ingawa mwandishi ametumia vivuli katika kazi yake, vivuli hivi katika dondoo vimetumika kuwakilisha hali halisi ya maisha ambapo wanawake wanadhulumiwa kwa sababu ya jinsia yao. Wanawake hawapewi nafasi ya kupinga matendo ya kikatili kama aliyotendewa Hawa. Sheria nazo haziwatetei wala kuwalinda wanawake, hivyo kudhihirisha ukosefu wa haki na mshikamano katika jamii. Katika muktadha wa ubaadausasa, kisa hiki cha Hawa kinaonekana kuihakiki simulizi kuu inayohusiana na nafasi ya sheria za nchi katika kulinda na kutetea haki za raia wake, hasa wanawake. Kama zilivyo simulizi kuu nyingine katika muktadha wa ubaadausasasa, sheria inaonekana kushindwa kutekeleza jukumu lake la kulinda haki za raia wake. Ufariji kutoka kwa Bi. Mau na Nana unajitokeza kama simulizi ndogo au njia mbadala ya kuweza kutuliza kivuli cha Hawa.

Matumizi ya jini, vizuu na mizuka katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ni dhihirisho la umazingaombwe unaoenda kinyume na kaida za uhalisia. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa Bi. Mau alikuwa ameolewa na jini au ruhani (uk 174). Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI jini ni kiumbe asiyeonekana, asiye shetani wala pepo. Kwa hivyo jini sio kiumbe kinachoweza kuonekana kwa macho katika ulimwengu halisi. Aidha, tunaelezwa kuwa jini hili linamwezesha kupenya katika ulimwengu wa kiroho ambapo anaona na kuzungumza na vizuu na mizuka. Matumizi ya majini, vizuu na mizuka katika maisha ya Bi. Mau yanadhihirisha umazingaombwe unaoenda sambamba na uhalisia.

Uhalisia mazingaombwe vilevile unajitokeza wakati wahusika wafu wanahuishwa na kupewa uwezo wa kutenda kama binadamu halisi katika mazingira halisi. Kwa mfano, Bimkubwa aliyekuwa amekufa miaka kadha iliyokuwa imepita anamjia mtoto wake, Nana, aliyekuwa hai na kuonyesha mapenzi yake kwake, jinsi ambavyo angefanya kama angekuwa hai:

> …Bimkubwa mamake, ndiye aliyemjia bintiye Nana hapo alipoganda….Alikuja tu akaketi naye sako kwa bako, pachapacha. Akanyoosha mikono yake kumshika kichwa chake na kukiinamisha mpaka kikagusa midomo yake ambayo ilibusu kipaji chake…alimtazama Nana kwa muda mrefu huku yeye mama mtu akikifululiza kicheko kisichokatika. Baadaye, Bimkubwa alitoa ziwa lake lililojaa na kulitia kinywani mwa binti yake….Wakati huu mama mtu alikuwa kiumbe kamili: si maiti, si mzuka. Ni Bimkubwa aliye hai, kiumbe kamili kisicho na ishara ya ufu (uk. 284-285/9).

Kama tunavyoelezwa kwenye dondoo, Bimkubwa anamtokezea binti yake kama kiumbe halisi wala si kama mfu au mzuka. Anatenda kama binadamu wa kawaida anapoenda kuketi karibu na bintiye, anamshika kichwa na kumbusu, anacheka na hatimaye kumnyonyesha Nana. Tunaelezwa kuwa Bimkubwa anamjia Nana mara kadhaa katika hali hii. Kwa mfano, anamjia Nana na kumpongeza kwa kuupigania uhuru wake kama mwanamke (uk. 285), na wakati mwingine anamjia kumwonya dhidi ya kuolewa kutokana na dhuluma mbalimbali anazoweza kupatana nazo kama mwanamke katika ndoa (uk.286-289). Anamsimulia Nana kisa chake mwenyewe kuhusu dhuluma alizozipitia katika

maisha yake ya ndoa pamoja na mahusiano yake na wanaume mbalimbali. Uwezo huu wa wafu kuhuishwa na kuweza kutenda kama binadamu halisi katika mazingira halisi unadhihirisha umazingaombwe unaoandamana na uhalisia katika riwaya hii.

Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* vilevile imetumia mhusika wa ajabu mwenye umbo la binadamu. Hata hivyo, mhusika huyu ni kiwiliwili tu ambacho hakina kichwa, yaani ni kibutu mtu kama kinavyoitwa katika riwaya hii. Hata hivyo, kina uwezo wa kutenda kama binadamu wa kawaida:

> Tokeo lile la ajabu lilitokea siku ile [Nana] alipokuwa njiani kutoka kazini akizungusha usukani wa gari lake… Alipotazama kulia yake aliliona lile gari la *Rolls Royce*. Dereva wake kibutu cha mwili; kiwiliwili kilichobutuka kichwa. Hakuwamini Nana. Aliinama kupagusa kile kioo cha dirisha la gari yake. Naam kwenye dirisha la *Rolls Royce* lenye kioo cha kiza, aliona kibutu cha mtu. Na hapo hapo hicho kibutu cha mtu kilichokuwa kikendesha gari kilimpungia mkono Nana. *Nani yule? Miujiza gani ile?* Alijiuliza (*NZM* uk. 217).

Kwa kawaida, kichwa ni sehemu muhimu sana katika mwili wa binadamu. Katika kichwa kuna viungo muhimu vinavyotusaidia kuona, kusikia na kuzungumza. Aidha, ubongo wa binadamu hupatikana kwenye kichwa na hutuwezesha kufikiria na kufanya maamuzi. Kwa kifupi, kichwa huwa kama injini inayoendesha mwili wa binadamu, na bila kichwa uhai wa binadamu hukatika. Hivyo basi kiumbe anachokiona Nana ni cha ajabu kwani hata bila kuwepo na kichwa bado ki hai, kinaona, kinazungumza na kusikia, kuwapungia watu mkono na hata kuendesha gari. Isitoshe, inaonekana kuwa wakati mwingine kiumbe hiki hujitokeza kama kichwa kilichotengana na kiwiliwili, yaani kichwa kibutu kama anavyokiita Nana. Wakati kinajitokeza katika hali hii huwa kinajibadilishabadilisha na kuchukua sura za watu tofauti:

> Siku hizo zote, Nana alifanya upekuzi sana kukitafuta kile kichwa butu, lakini hakufanikiwa. Siku moja kwa miujiza, alikiona kimetokeza waziwazi kichwa hicho, kwa sura ya Mwarabu, ingawa hakuwa na hakika kama kilikuwa cha Mwarabu kweli au la. Baadaye, siku nyingine, kichwa kilitokeza kwa wasifu wa Mjerumani. Pia hakuweza kusema kwa asahi kama kilikuwa cha Mjerumani au Mchina au Mhispania. Kuna siku kilijitokeza kwa sura ya Mwingereza aliyevaa shati la bendera ya Kiingereza. Kisha siku nyingine cha Mmarekani aliyejizonga kanda la *Cow Boy* shingoni. Kisha ikaja sura ya mtu mweusi. Na mwisho kichwa kikawa cha Mwitaliano kabla hakijageuka Kaburu wa Afrika ya Kusini. Jambo hili sasa halikumshangaza tu Nana, lilimpa hofu. … Nani huyu kiumbe anayejigeuzageuza kama kinyonga? Anayeanza kwa kitendawili cha ubutu na kuishia kubadilisha nyuso? (*NZM* uk. 218).

Ingawa kiumbe hiki kinajitokeza kama mazingaombwe, kinaashiria matukio halisi katika ulimwengu halisi. Kama anavyosema Baldick (2008) sifa za uhalisia mazingaombwe hutumiwa kutoa taswira ya jumla ya mabadiliko ya kisiasa katika karne ya 20. Tunaweza kusema basi kuwa sura mbalimbali za kiumbe hiki zinaashiria aina tofauti ya wakoloni na ukoloni katika Afrika na maeneo mengineo ulimwenguni kote yaliyotokea kabla na baada ya karne 20. Hivyo basi, tunarejelea ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Katika karne hii ya 21 tunatawaliwa na ukoloni mamboleo ulio na msingi wake katika ukoloni mkongwe. Kutawaliwa huku hakujitokezi wazi wazi bali kumejificha na kunaendelea kuwaathiri watu hasa walio katika mataifa ya ulimwengu wa tatu. Hii ndio maana kiumbe hiki kinajitokeza kama kiwiliwili kibutu ili kuuficha uso wake kuashiria ukoloni ambao bado upo lakini kwa njia ilyofichika. Ukoloni mamboleo bila shaka umesababisha ukosefu wa mshikamano katika jamii. Kama mhusika kwenye kazi ya kifasihi, matumizi ya kibutu mtu na uwezo wake wa kubadilishabadilisha sura unakiuka uwezo wa binadamu wa kawaida, na hivyo kuonyesha mabadiliko katika utanzu huu wa riwaya yanayokaidi uandishi wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia.

**HITIMISHO**

Makala haya yamejadili uhalisia mazingaombwe kama kipengele mojawapo cha mtindo katika riwaya za kibaadausasa. Imebainika kuwa uhalisia

mazingaombwe ni mtindo wa uandishi unaokiuka kaida za kihalisia zilizokuwa zimezoeleka na kutumiwa na wanamapokeo kama msingi wa kuifafanua riwaya. Badala yake riwaya za kibaadausasa zinatumia uhalisia unaoenda sambamba na umazingaombwe. Matumizi ya mtindo huu ni dhihirisho la upya katika fasili ya riwaya inayopinga fasili ya awali na kudhihirisha njia anuwai za kujieleza bila kufungwa na simulizi kuu ya wanamapokeo. Aidha, mtindo huu umetumika kuwakilisha ulimwengu wa sasa uliojaa mambo mengine ya ajabu ambayo yamesababisha kutokuwepo na mshikamano katika jamii.

**MAREJELEO**


Baldick, C. (2008). *Oxford Dictionary of Literary Terms*. Oxford University Press.

Bowers, M. A. (2004). *Realism*. Routledge.

Barry, P. (2002). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. Manchester University Press.

Baudrillard, J. (1981). *Simulacra and Simulation*. University of Michigan Press.

Deleuze, G., & Guattari, F. *Anti-Oedipus:* (1972). Kimetafsiriwa na Hurley, R., Seem, H. M. & Lane, H. R. (1983). The Athlone Press.

D'haen, T. L. (2005). Magical Realism and Postmodernism: Decentreing Privileged Centres. Katika: Zamora, L. P., & Faris W. B. (1995) (whr). *Magical realism: Theory, History, Community*. Duke University Press.

Forster, E. M. (2002). *Aspects of the Novel*. RosettaBooks LLC.

Goring, P., Hawthorn, J., & Mitchell, D. (2010). *Studying Literature (2nd Edition)*. Bloomsbury Publishing PLC.

Khamis, S. A. M. (2005). Signs of New Features in the Swahili Novel. *Research in African Literatures, 36*(1), 91-108. Indiana University Press.

Khamis, S. A. M. (2007). The Swahili Novelist at the Crossroad: The Dilemma of Identity and Fecundity. *Swalihi Forum, 14*: 165-180.

Khamis, S. A. M. (2008). Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na Taaluma ya Kiswahili. Katika: N. O. Ogechi, N. L. Shitemi & K. Simala. *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Moi Univresity Press.

Lewis, B. (2001). Postmodernism and Literature. Katika: Sim S. (mhr) (2001). *The Routledge Companion to Postmodernism.* Routledge.

Lyotard, J. F. (1979). *The Postmodern Condition: A Report on Knowledge*. Kimetafsiriwa na Bennington, G., & Massumi, B. (1987). Manchester University Press.

Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mwamzandi, I. Y. (2013). Riwaya za Karne ya 21 na udurusu wa nadharia za Fasihi. *Swahili Forum, 20,* (48-66).

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Kifasihi*. Tasnifu ya Ph.D. (Haijachapishwa).

Pollheide, J. (2003). *Postmodernist Narrative Strategy in the Novels of John Fowles*. Tasnifu ya Ph.D. Bielefed University (Haijachapishwa).

Rivkin J., & Ryan, M. (2004). *Literary Theory – An Anthology* (Second Edition). Blackwell Publishing.

Salenius, C. (2009). *From the Margins to the Mainstream: Magical realism and Feminism in Alice Hoffman's 'Practical Magic' and Joanne Harns's 'Chocolat'*. Tasnifu ya MA, University of Tampere (Haijachapishwa).

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam. KAUTTU.

Sim, S. (2001). *The Routledge Companion to Postmodernism*. Routledge.

Traore, F. A. (2015). Postmodernism as seen through the Swahili Novel: A reading of *Babu Alipofufuka* and *Dunia Yao* by Said Ahmed Mohamed. Katika: *Journal of African Cultural Studies, 27*(1): 20-29.

Waliaula, K. W. (2010). Uhalisia na Uhalisia mazingaombwe: Mshabaha kati ya *Dunia Yao* na *The Tin Drum*. *Swahili Forum*, *17*: 143-157.
Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Phoenix Publishers Ltd.
Watt, I. (2000). *The Rise of the Novel: Studies in Defoe, Richardson and Fielding*. PIMLICO.
Zamora, L. P., & Faris W. B. (1995). *Magical realism: Theory, History, Community*. Duke University Press.